Jarida la Wizara ya Afya

# Afya Habari

JARIDA LA MTANDAONI LA WIZARA YA AFYA | TOLEO, NO. 14, DISEMBA 2023






# TUNABORESHA AFYA

MTU NI AFYA, JALI AFYA YAKO




## BODI YA UHARIRI

**MWENYEKITI**
Dkt. John Jingu
KATIBU MKUU

**MHARIRI**
Englibert Kayombo

**MHARIRI MSAIDIZI**
Emmanuel Malegi

**WAJUMBE**
Englibert Kayombo
Emmanuel Malegi
Majid Abdulkarim
Said Nyaoza
Hassan Kimweri
Shaban Juma
Cletus Sanga
Abdulwaheed Madenge

**WASANIFU**
Englibert Kayombo
Said Nyaoza

@wizara_Afyatz
www.moh.go.tz

# YALIYOMO



Hanang chukueni tahadhari dhidi ya magonjwa ya mlipuko-dkt. Samia....UK 1



Hongera Wizara ya Afya kwa kuongeza wataalamu wa upasuaji kwa majeruhi wa maafa ya Katesh.... UK 2




Uzalishaji wa dawa nchini utasaidia upatikanaji wa dawa kwa wakati na gharama nafuu.... UK 3



Maambukizi ya VVU kwa watu wazima yapungua..... UK 4



Asilimia 81 ya wajawazito wanajifungua katika vituo vya kutoa huduma za afya.... UK 5



Mabadiliko ya tabia nchi yasababisha kuongezeka kwa magonjwa ya milipuko nakuathiri mfumo wa utoaji huduma za afya..... UK 7



Waziri ummy aitaka ocean road kuanza kutumia pet-ct scan ndani ya mwezi mmoja.... UK 8



Doris Mollel Foundation yatoa vifaa tiba kwa ajili ya kuanzisha wodi ya watoto wachanga .... UK 9



Zaidi ya familia 760 hanang zapatiwa elimu ya kujikinga na magonjwa ya mlipuko. .... UK 10



Rais samia kuendelea kuimarisha huduma za afya mipakani .... UK 12



Rais Samia achangia taasisi ya Prof. Jay shilingi Milioni 97... UK 13



Tusiwafiche watoto wenye Usonji- Dkt. Mollel .... UK 16



Rais Samia kuwezesha wananchi wengi kufikiwa na huduma za kibingwa na bingwa bobezi .... UK 17



Wananchi zingatieni kanuni za afya kujikinga na magonjwa ya mfumo wa hewa.... 18



Tanzania yavunja rekodi matibabu ya Moyo.... UK 19



Wizara ya Afya kushirikiana na JICA kuimarisha huduma za Afya ya uzazi, mama na mtoto .... UK 20



Wabunifu wa huduma za afya za kidigitali wahimizwa kuboresha huduma bora za afya kupitia tehama .... UK 21



MSD itoe huduma za mnyororo wa ugavi wa bidhaa za afya kwa wateja wao - Dkt. Jingu.... UK 22



Wizara ya afya yakutana na wadau wa sekta ya afya, yawapitisha kwenye sheria ya mfuko wa bima ya afya kwa wote.i..... UK 23



Umoja wa wamiliki vituo binafsi vya afya (APHTA), wapitishwa kwenye sheria ya bima ya afya kwa wote .... UK 24



Mtambo wa kutibu magonjwa zaidi ya 10 wazinduliwa Muhimbili.... UK 25



Muhimbili yapeleka msaikolojia tiba katesh na msaada wa dawa za tzs. 38 mil.... UK 26




# Hanang chukueni tahadhari dhidi ya magonjwa ya mlipuko - Dkt. Samia

**Na Englibert Kayombo,**
**Hanang, Manyara**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa wito kwa wananchi Mji mdogo wa Katesh Wilaya ya Hanang Mkoani Manyara na Watanzania kwa ujumla kuendelea kuchukua tahadhari za magonjwa ya mlipuko kwa kuchukua hatua za matumizi ya maji safi na salama.

Dkt. Samia alitoa wito huo wakati akizungumza na wananchi mji mdogo wa Katesh Wilayani Hanang Mkoa Manyara baada ya Disemba 3, 2023 kukumbwa na maafa ya mafuriko yaliyosababisha maporomoko ya udongo kutoka mlima Katesh na kusababisha madhara makubwa ikiwemo majeruhi,vifo na upotevu wa mali.

"Jambo kama hili linapotokea huwa yanatokea magonjwa ya mlipuko, niwaombe wananchi wachukue hatua stahiki za kuzingatia kanuni za afya pindi wanapotumia maji wazingatie kuepuka magonjwa ya mlipuko ikiwemo kuhara "alisema.

Aidha, Rais Samia alitoa maagizo kwa Wizara ya Afya kuhakikisha elimu na ufuatiliaji kwa kina inatolewa kwa wananchi.

"Wizara ya Afya hakikisheni elimu juu ya kujikinga na madhara yanayoweza kutokea kutokana na mafuriko inatolewa pia kufuatilia kwa kina majeruhi mpaka kuhakikisha wanakuwa katika hali ya kawaida"alisema Dkt Samia.

Halikadhalika, Dkt.Samia aliagiza kuhakikisha msaada wa Kisaikolojia unaendelea kutolewa pamoja na huduma za maji safi na salama kuendelea kuimarishwa.

Hata hivyo, alitumia fursa hiyo kuwashukuru wadau kwa kutoa msaada ambapo jumla ya Tsh.Bilioni 2.5 zimetolewa na wadau kutoka nje ya nchi huku akielekeza zitumike kujenga makazi ya kudumu kwa waathiriwa.



# Hongera Wizara ya Afya kwa kuongeza wataalamu wa upasuaji kwa majeruhi wa maafa ya Katesh

**Na. Majid Abdulkarim,**
**Hanang, Manyara**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa alii-pongeza Wizara ya Afya kwa jitihada za kuongeza wataalamu wa upasuaji katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara kwa ajili ya kuhudumia majeruhi wa maafa ya mafuriko yaliyotokea Katesh Wilayani Hanang.

Mhe. Majaliwa alibainisha hayo wakati alipowasili wilaya ya Hanang mkoani Manyara na kukutana na viongozi wa mkoa huo na wa Serikali na kupokea taar-ifa ya hali halisi ya tukio la maafa lililo-tokea Disemba 3, 2023 na kusababisha vifo na majeruhi.

Waziri Mkuu alitoa pole kwa viongozi na wananchi wa Hanang kwenye kikao kili-chofanyika kwenye ukumbi wa Hal-mashauri ya Wilaya ya Hanang na kuhud-huriwa na viongozi mbalimbali wakiwe-mo Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, vyombo vya ulinzi na usalama na Watendaji wa taasisi za Serikali.

Mhe. Majali alisema kuwa tukio la Katesh linafanana na tukio jingine lililowahi kutokea mwaka 1990 katika eneo la Ndanda ambako mlima uliporomoka na kusomba nyumba na barabara, hali ambayo ilisababisha vifo na majeruhi.

Alizishukuru Kamati za Maafa za Wilaya na Mkoa ambazo zilianza kuchukua hatua za uokoaji tangu tukio hilo litokee, lakini pia Mawaziri na watendaji wao ambao waliji-tokeza kutoa msaada kwa kuungana na viongozi wa mkoa wa Manyara.

Alisema matibabu yanaendelea kutolewa kwa majeruhi ambapo timu ya madaktari bingwa kutoka Dodoma, Singida na Arusha ziliungana na kuanza kutoa huduma za upasuaji kwa wagonjwa watatu waliovunjika mifupa.

Alisema majeneza yaliagizwa kutoka Babati na Singida ili ndugu waliotambuli-wa waweze kuhifadhiwa kwenye nyumba zao za milele.

hatua nyingine Mhe. Majaliwa na baadhi ya mawaziri walikwenda kukagua eneo la mlima Hanang kwa kutumia helikopta, eneo ambalo maporomoko ya udongo yalianzia. Ambapo pia aliweza kushiriki tukio la kuaga miili ya marehemu na taar-ifa rasmi ilitolewa .





# Uzalishaji wa dawa nchini utasaidia upatikanaji wa dawa kwa wakati na gharama nafuu

**Na Cletus Sanga,**
**Dar es Salaam**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alitoa rai kwa Wadau wa Maendeleo kuunga mkono jitihada za Serikali kwa kuwekeza zaidi nchini kwenye Sekta ya Afya huku wakiiga mfano wa Kampuni ya uzalishaji wa Dawa cha Cure Afya ambayo iko mbioni kuanza uzalishaji wa dawa hapa hapa nchini.

Waziri Ummy aliyasema hayo alipo tembelea Kiwanda kipya cha utengenezaji Dawa cha Cure Afya ambacho kipo Wilaya ya Kigamboni Jiijini Dar Es Salaam kwa ajili ya kuona utayari wa Kiwanda hicho kutengeneza Dawa kwa ajili ya soko la ndani ya nchi pamoja na nchi jirani.



"Dawa zinazozalishwa zitarahisisha upatikanaji wake kwa wakati, tofauti na tukiagiza dawa nje ya nchi zinachukua miezi 6 hadi 9 kuweza kufika hivyo inachukua muda mrefu mpaka kufika nchini". Alisema Waziri Ummy.

Alisema serikali imejizatiti kukuza uzalishaji wa dawa wa ndani ili kupunguza gharama ya uagizaji kwani Tanzania ni miongoni mwa nchi nne za Afrika ambazo zinatambulika kwa umahiri kupitia Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba TMDA na Shirika la Afya Duniani WHO.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Cure Afya Bw. Paresh Ghelani alisema kuwa wako tayari kwa uzalishaji wa dawa kuanzia Januari 2023 ikiwa ni takwa la Serikali katika uwekezaji wa viwanda kwa mahitaji ya nchi ambayo yatakwenda kurahisisha upatikanaji wa dawa kwa wakati na gharama nafuu.

Haya ni matokeo chanya ya uhamasishaji Fursa za Uwekezaji wa Viwanda nchini yanayofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo ya Sekta ya Afya nchini katika kuendelea kuboresha Sekta ya Afya nchini na kuifanya Tanzania kuwa Kituo cha Utalii tiba ukanda wa Afrika Mashariki.

# Tusiwafiche watoto wenye Usonji- Dkt. Mollel




**Na Majid Abdulkarim**
**Dar Es Salaam.**

Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel alitoa wito kwa wananchi kutowaficha watoto wenye changamoto ya Usonji (Autism) kwani wakipata malezi na mafunzo mazuri watasaidia kuleta matokeo chanya katika jamii.

Dkt. Mollel alisema hayo wakati akifungua Mkutano wa kimataifa wa Usonji (Autism) uliofanyika katika kituo cha kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam.

Alisema, katika kusaidia kupambana dhidi ya changamoto hiyo, Rais Samia alipoingia madarakani aliongeza bajeti ya Wizara ya Afya mpaka kufikia Trilioni 6.7 iliyosaidia kununua MRI kwenye hospitali za Kanda na CT-SCAN katika hospitali zote za Rufaa za Mikoa zitazosaidia katika kugundua magonjwa mbalimbali ikiwemo Autism.

Aliendelea kusisitiza kuwa, kupitia mpango wa Dkt. Samia Health Specialisation Programu tayari Dkt. Samia alitoa Bilioni 9 kwaajili ya kupeleka Wataalamu wa Afya wasiopungua 300 nje ya nchi ili kupata ujuzi wa fani za kibingwa na ubingwa bobezi na kusisitiza mpango huu ni endelevu.

Sambamba na hilo, Dkt. Mollel alisema, tatizo la usonji (autism) linaendelea kuongezeka nchini na Duniani kwa ujumla, huku akisema mwaka 2021 katika kila watoto 44 mtoto mmoja alikuwa na changamoto ya autism lakini kwa mwaka 2023 katika kila watoto 36 mtoto mmoja ana Autism.

Aidha, Dkt. Mollel alisema, watoto wenye changamoto ya Usonji (autism) wanatakiwa uangalizi wa karibu na kukuza vipaji ili vyao vya uvumbuzi, ili kuleta tija katika jamii.

"Kuna wanasayansi wakubwa Duniani ambao wamegundua mambo mbalimbali na binadamu wakayafurahia, baadhi yao walikuwa watoto wenye changamoto kama hii ya Usonji (autism)." Alisema Dkt. Mollel.



# Maambukizi ya VVU kwa watu wazima yapungua

**Na. Shaban Juma**
**Dar es Salaam**

Utafiti wa hali ya UKIMWI nchini (Tanzania HIV Impact Survey - THIS 2022/23) umeonyesha kiwango cha maambukizi ya UKIMWI kwa watu wazima (miaka 15 na zaidi) kuwa kimepungua kutoka asilimia 4.9 mwaka 2016/17 hadi asilimia 4.4 mwaka 2022/23.

Mikoa mitatu yenye kiwango cha juu cha maambukizi katika utafiti huu ni Njombe (12.7%), Iringa (11.1%) na Mbeya (9.6%), na mikoa yenye maambukizi ya chini ni Kigoma (1.7%), Manyara (1.8%) na Lindi (2.6%).

Kwa utafiti wa mwaka 2016/17, mikoa iliyoongoza kwa kiwango kikubwa cha maambukizi ilikuwa ni Njombe (11.4%), Iringa (11.1%) na Mbeya (9.3%). Mikoa iliyokuwa na maambukizi ya chini ilikuwa ni Kigoma (2.9%), Manyara (2.3% na Lindi (0.3%).

Katika kufikia malengo ya 95-95-95 ifikapo mwaka 2025, kiwango cha watu wanaofahamu hali yao ya maambukizi kuhusu VVU ni asilimia 82.7 kwa 2022/23 kulinganisha na asilimia 60.6 kwa mwaka 2016/17,

kiwango cha watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi (WAVIU) na wanatumia dawa za kufubaza VVU (ARV) ni asilimia 97.9 kulinganisha na asilimia 93.6 mwaka 2016/17. Aidha, kiwango cha wanaotumia dawa na wamefubaza VVU ni asilimia 94.3 mwaka 2022/23 kulinganisha na asilimia 87 mwaka 2016/17.

“Nitumie fursa hii kumshukuru kwa dhati Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuwezesha kufikia mafanikio haya ikiwemo kuhakisha huduma bora za tiba na matunzo kwa WAVIU. Aidha nimamshukuru Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa kwa kutuongoza vyema katika mapambano dhidi ya Ukimwi” alisema Waziri Ummy Mwalimu.

“Nawashukuru viongozi na wataalam wote wa sekta ya Afya nchini kwa kujitoa kwao katika mapambano dhidi ya Ukimwi ikiwemo kuwahudumia WAVIU. Ninayashukuru mashirika ya kiraia kwa kazi nzuri. Kipekee ninawashukuru wadau wetu hususani CDC’s Global, CDC’s Tanzania, Global Fund, PEPFAR, USAID Tanzania na UNAIDS kwa kuchangia rasilimali fedha na utaalamu katika mapambano dhidi ya Ukimwi. Asanteni sana wananchi kwa kushiriki vita hii. Ninaomba tuendee kuchukua hatua ili kujikinga na VVU na endapo tayari una maambukizi basi usiache kutumia dawa za ARVS. Kwa pamoja tunaweza kutokomeza Ukimwi nchini Tanzania”. AlisemA



# Wizara ya Afya kushirikiana na JICA kuimarisha huduma za Afya ya uzazi, mama na mtoto

**Na Shaban Juma**
**Dar Es Salaam**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu alikutana na Shirika la Kimataifa la Ushirikiano la Japan JICA kujadili namna ya kuboresha huduma bora za Afya kupitia mradi wa kuimarisha Huduma ya Afya na matunzo ya uzazi na watoto wachanga.

Hayo yalijiri katika kikao kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Afya zilizopo jijini Dar es salaam ambapo pia Dkt. Jingu aliwashauri katika kuboresha huduma za afya

Aidha Dkt. Jingu alilishauri shirika hilo katika kuboresha huduma za Afya ni vyema kuboresha mafunzo kwa Wahudumu wa Afya katika utoaji bora wa Huduma bora ili iweze kuimarisha Huduma za Afya katika vituo vya kutolea huduma za Afya nchini.

"Tunatakiwa kuwajengea mafunzo wahudumu wetu wa Afya katika maeneo tofauti tofauti ili kuweza kuimarisha Huduma hii ya mama Mjamzito na watoto wachanga ili kuendelea kuboresha Huduma bora kwa mama na mtoto". Alisema Dkt. jingu

Pia, Dkt. Jingu alilishauri shirika hilo katika kuendelea kuboresha miundombinu ya mama wajawazito na watoto wachanga na kujenga miundombinu katika maeneo ambayo hayana ikiwemo kitengo cha utunzaji mkubwa wa watoto wachanga (NICU) na jengo la Uzazi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Tiba anaesimamia Hospitali za Rufaa za Mikoa Dkt. Caroline Damian alisema Serikali kupitia Wizara ya Afya imedhamiria kuwa na vituo sita vya ubora wa Huduma za Afya ya Uzazi na Watoto Wachanga nchini.



# Asilimia 81 ya wajawazito wanajifungua katika vituo vya kutoa huduma za afya



**Na Said Nyaoza**
**Dodoma**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alisema asilimia 81 ya wajawazito nchini wanajifungulia katika vituo vya kutoa huduma za Afya ukilinganisha na asilimia 63 kwa mwaka 2016.

Waziri Ummy alisema hayo Disemba 18, 2023 kwenye ukurasa wake wa X wakati akifafanua juu ya upotoshaji unaondelea katika mitandao ya kijamii kuhusu wajawazito kujifungulia chini.

“Ukweli utabaki kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imewekeza sana katika kuboresha huduma za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto ambapo kwa sasa asilimia 81 ya wajawazito nchini wanajifungulia katika vituo vya kutoa huduma za Afya.” Alisema Waziri Ummy
Aidha Waziri Ummy alisema vifo vya wajawazito vimepungua kutoka vifo 556 katika kila vizazi hai laki 100,000 hadi vifo 104 katika kila vizazi hai laki 100,000, namba zinaongea.

Akiendelea kufafanua malalamiko hayo Waziri Ummy alisema katika Sekta ya Afya kila siku zinaibuka changamoto mpya hivyo haiwezekani kumaliza changamoto zote kwa siku moja au muhula mmoja.

“Tutaendelea kuchukua hatua mahususi ili kuzitatua kwa haraka changamoto za utoaji huduma za Afya nchini kadri zinavyojitokeza Serikali ya Rais Samia inazipa kipaumbele cha hali ya juu huduma za Afya ya Uzazi, mama na mtoto.





# Wizara ya afya yakutana na wadau wa sekta ya afya, yawapitisha kwenye sheria ya mfuko wa bima ya afya kwa wote

**Na. Emmanuel Malegi**
**Dar Es Salaam**

Wizara ya Afya kupitia Naibu Katibu Mkuu Dkt. Grace Magembe pamoja na wataalam wamekutana na Wadau wa Maendeleo ya Sekta ya Afya nchini na kujadili namna wanavyoweza kushirikiana katika utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ambao hivi karibuni ilisainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza wakati wa kufungua kikao kazi hicho, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. Grace Magembe alisema wadau hao ni muhimu katika sekta hivyo wanaguswa moja kwa moja katika utekelezaji wa Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote na muhimu kukutana kwa pamoja na kuweza kuipitia Sheria hiyo, itakayowaongoza katika utekelezaji.

Kwa upande wake mwakilishi wa Wadau wa Maendeleo katika Sekta ya Afya, ambaye pia ni Mwakilishi kutoka Ubalozi wa Uingereza Bi.Gertude Mapunda, alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt Samia Suluhu kwa kuweza kusaini na kukubali Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote kuanza kutumika nchini na kuahidi kuwa Wadau wa maendeleo wapo tayari kushirikiana na Serikali katika kufikia azma ya Bima ya Afya kwa Wote.

“Kuja kwa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote itakuwa ni msaada mkubwa kwa Watanzania walio wengi, kwani kutokana na unafuu wake utasaidia wengi kujiunga na kuwa wanachama na kufanikisha upatikanaji wa huduma za Afya kuwafikia walio wengi” Alisema Bi Getrude.

Katika kikao hicho Wadau wa Maendeleo katika Sekta ya Afya walifanikiwa kupitishwa kwenye Sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote, namna mfuko huo utakavyotekelezwa na pia walipata wasaa wa kujadiliana masuala mbalimbali yatakayojitokeza pindi mfuko huo utakapoanza kutekelezwa.

# Rais Samia achangia taasisi ya Prof. Jay shilingi Milioni 97

**Na. Majid Abdulkarim,**
**Dar Es Salaam**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan iliahidi kuchangia kiasi cha shilingi milioni 97 katika taasisi ya Profesa Jay Foundation yenye lengo la kuisaidia Jamii matibabu ya ugonjwa wa figo.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel katika uzinduzi wa taasisi hiyo akimwakilisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa iliyofanyika katika ukumbi wa Mlimani City Jijini Dar es Salaam.

Akifafanua mchango huo wa Serikali kwenda kwenye Taasisi ya Profesa Jay Dkt. Mollel alisema Tshs Mil. 50 zitakwenda moja kwa moja kwenye Taasisi na Tshs. Mil. 47 ni kwa ajili ya matibabu ya Prof. Jay ikiwa atahitaji kupandikiza figo.

Aidha, Dkt. Mollel alibainisha gharama ya Upandikizaji figo ni Mil. 47 hivyo kufikisha jumla ya milioni 97 ikiwa lengo ni kuimarisha Afya za Watanzania.

Hata hivyo katika uzinduzi huo Dkt. Mollel aliwasilisha ahadi ya Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa katika taasisi ya Profesa Jay ikiwa ni shilingi Mil. 10.

Pia, Dkt. Mollel aliwaasa watanzania kuona umuhimu wa kuwa na Bima ya Afya kwani Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa ili kupunguza gharama za matibabu na kuboresha Huduma za Afya.





# Mabadiliko ya tabia nchi yasababisha kuongezeka kwa magonjwa ya milipuko nakuathiri mfumo wa utoaji huduma za afya.

**Dubai**

Waziri wa Afya Ummy Mwalimu alishiriki katika kikao cha Mabadiliko ya tabia nchi na Afya ngazi ya Mawaziri wa Afya kutoka nchi wanachama wa Shirika la Afya Duniani. Kikao hiki kilichotoa umuhimu wa suala la Afya kilifanyika pembezoni mwa kikao cha 28 cha Duniani kuhusu mabadiliko ya tabia nchi.

Waziri Ummy aliuambia mkutano huu kwamba, mabadiliko ya tabia nchi, yamesababisha ongezeko la magonjwa ya milipuko na vifo hususani katika nchi za Afrika zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara. Mathalani, magonjwa kama kuhara, malaria, dengue na magonjwa yasiyopewa kipaumbele kama usubi, chikungunya, kichocho, matende na magonjwa ya mfumo wa hewa, magonjwa ya aina hii yanatarajiwa kuongezeka kutokana na ongezeko la joto na mvua kubwa au chache zinazoletelezea mafuriko au ukame katika maeneo mbalimbali nchini.

Waziri Ummy alitolea mfano wa mafuriko yaliyotokea nchini mkoani Manyara na kupoteza maisha ya watu na wengine kujeruhiwa. Majanga kama ya mafuriko yameonekana kusababisha milipuko ya magonjwa ikiwemo kipindupindu na Homa ya matumbo na kueleza kuwa asilimia 88 tu ya wakazi wa mijini ndiyo wanaopata huduma ya maji safi na salama na kwa upande wa vijijini ni asilimia 77 na watu wenye vyoo vya aina yoyote ni asilimia 98.

“Aidha majanga kama ya mafuriko yamepelekea kuharibu vyanzo vya maji na miundombinu iliyopo na kupelekea upungufu na hatimaye milipuko ya magonjwa." Alisema Waziri Ummy

Tanzania kama moja ya nchi zinazoathirika na mabadiliko ya tabia nchi inaendelea kuchukua hatua za makusudi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kuandaa mpango mkakati na miongozo ya kukabiliana na majanga haya katika sekta ya Afya.

Vile vile Wizara iliandaa mfumo wa taarifa unaoweza kubashiri uwezekano wa kutokea milipuko ya magonjwa sambamba na mabadiliko ya hali ya hewa ya kila siku. Aidha alieleza kuwa Wizara inatafuta fedha za kutekeleza Afua mbalimbali za kukabiliana na kuhimili mabadiliko ya tabia nchi kwa ushirikiano na mashirika ya kimataifa yanayojishughulisha na mazingira, Afya na maendeleo ya jamii.



# Wananchi zingatieni kanuni za afya kujikinga na magonjwa ya mfumo wa hewa

**Na. Emmanuel Malegi**
**Dodoma**

Mganga mkuu wa Serikali Prof. Tumaini Nagu amewataka wananchi kuzingatia kanuni za afya kwa kuzingatia usafi na kupata chanjo ya UVIKO 19 kwa ukamilifu ili kujikinga na magonjwa ya njia ya hewa ikiwemo mafua, kikohozi, kupumua kwa shida, kuwashwa koo, homa na kuumwa kichwa.

Prof. Nagu aliyasema hayo kufuatia tetesi za kuongezeka kwa magonjwa ya mfumo wa njia ya hewa ambapo alisema magonjwa ya mfumo wa hewa yapo muda wote Nchini huku akibainisha kwamba kumekuwepo na vipindi vya kuongezeka na kupungua kwa visa hivi kwa nyakati tofauti katika mwaka.

Aidha Prof. Nagu alisema Wizara imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa taarifa za magonjwa ya mlipuko ikiwa ni pamoja na tetesi za kuwepo kwa magonjwa hayo ndani na nje ya Nchi ambapo kuanzia November, 2023 kumekuwa na tetesi juu ya ongezeko la visa vya magonjwa ya mfumo wa njia ya hewa sehemu mbalimbali duniani na ndani ya nchi hususan Dar es salaam ambapo alisema UVIKO19 umeendelea kuwepo kwa kiwango cha chini kama magonjwa mengine ya mfumo wa njia ya hewa ukiongezeka na kupungua kwa nyakati tofauti za majira ya mwaka.

Prof. Nagu alisema virusi vya Influenza vilivyobainika nchini havina madhara makubwa ndio maana unaitwa Ugonjwa wa Majira (Seasonal Influenza) lakini hata hivyo takwimu za ufualitiliaji (Surveilance) za Wizara zinaonesha ongezeko la maambukizi ya Uviko 19 kutoka 37 mwezi October 2023 hadi maambukizi 65 mwezi December 2023"

"Aidha, ongezeko hili ni sambamba na ongezeko la maambukizi ya mafua yanayotokana na influenza kutoka maambukizi 34 hadi 49 katika kipindi hicho hicho". Alisema Prof Nagu.

Wizara inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa magonjwa ya mfumo wa njia ya hewa na inaelekeza Wataalamu katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya kuendelea kufanya utambuzi kwa njia ya vipimo vya maabara na kutoa matibabu stahiki, huku ikiwashauri Wananchi kuwahi kwenye Vituo vya kutolea huduma mara wapatapo dalili za magoniwa ya mfumo wa njia ya hewa zikiwemo mafua, kikohozi, kuwashwa koo, kupumua kwa shida, homa na kuumwa kichwa.

# MSD itoe huduma za mnyororo wa ugavi wa bidhaa za afya kwa wateja wao - Dkt. Jingu

**Na. Abdulwaheed Madenge**
**Morogoro**

Katibu Mkuu Wizara ya Afya Dkt. John Jingu aliielekeza Bohari ya Dawa (MSD) kuwajali Wateja na kuwashirikisha katika suala zima la kuwapa huduma za mnyororo wa ugavi wa bidhaa za Afya nchini.

Dkt. Jingu alisema hayo wakati akifungua kikao cha ishirini na mbili (22) cha baraza la Wafanyakazi la MSD Mkoani Morogoro ambapo alisisitiza kuwa, kujali wateja ni msingi wa kuwahudumia kulingana na mahitaji yao.

"Ni muhimu sana kuwajali wateja wetu na tuwashirikishe katika suala zima la kuwapa huduma za mnyororo wa ugavi wa bidhaa za Afya nchini ili wajue kazi inayofanywa na Serikali." Alisema Dkt. Jingu

Aidha, Dkt. Jingu alisisitiza umuhimu wa MSD kujiendesha kibiashara na kuwa wabunifu ili kuweza kuleta ufanisi na tija katika jamii.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa MSD Bw. Mavere Tukai alisema kuwa MSD ni miongoni mwa Taasisi za kimkakati na imeanza kujiendesha kibiashara.

"Katika kipindi cha mwaka mmoja, MSD imeweza kuongeza hali ya upatikanaji wa bidhaa za Afya kwa kuingia mikataba ya muda mrefu na wazalishaji ambapo upatikanaji wa dawa umeongezeka kutoka 51% mwaka jana wa fedha, hadi kufikia zaidi ya 80% mwaka huu." Alisema Bw. Tukai

Alisema, eneo hili pia linaonekana kwenye kutimiza mahitaji ya wateja ambapo mwaka jana ilikuwa ni asilimia 44 na hii imeongezeka na kufikia asilimia 78.

Kwa upande wa mauzo, Tukai alisema kuna ongezeko la mauzo ya bidhaa za Afya kutoka shilingi Bilioni 77 mwaka jana wa fedha na kufikia shilingi Bilioni 123 mwaka huu wa fedha.

"MSD itaendelea kuboresha kazi zake kwa kuimarisha utendaji wa kazi zake ili kuendelea kutoa huduma za upatikanaji wa bidhaa za Dawa kwa Watanzania." Alisema Bw. Tukai



# Waziri Ummy aitaka ocean road kuanza kutumia PET-CT SCAN ndani ya mwezi mmoja

**Na. Cletus Sanga,**
**Dodoma**

Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alizitaka Taasisi ya Saratani Ocean Road hadi kufikia Fubruari Mosi, 2024 mashine ya Pet-CTScan iwe imeanza kutoa huduma kwa Watanzania ili rufaa za kwenda nje ya nchi zipungue.

Waziri Ummy alitoa tamko hilo baada ya kufanya ziara ya kujionea huduma zinazotolewa katika Taasisi ya Saratani Ocean Road jijini Dar es Salaam.

"Mmeniambia tarehe 26, Disemba mtafanya majaribio ya mashine hii sasa nataka nikija tena hapa tarehe 01-02-2024 nione mashine ya Pet-CT Sacan iwe imeanza kufanya kazi Ili Watanzania waweze kupata huduma za Pet-Ct Scan hapa nchini." Alisema Waziri Ummy

Aidha, Waziri Ummy alimshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kujali Afya za  Watanzania kwa kuipa fedha Sekta ya Afya kwa ajili ya matibabu ikiwemo ya Saratani pamoja na vifaa Tiba.

Alisema, kwa sasa wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi kwa udhamini wa Serikali ni wagonjwa  42 wakiwemo wa Saratani wagonjwa 15 kwa muda wa miezi mitatu kuanzia Julai hadi Septemba  mwaka huu.

"Tunataka kupunguza Rufaa za nje ya nchi ili kusogeza huduma kwa Watanzania lakini pia kuokoa fedha za Serikali na tutaendelea kuwekeza katika kuboresha huduma za Saratani nchini." Alisema Waziri Ummy

Pia, Waziri Ummy aliitaka Taasisi ya Saratani Ocean Road kwenda kuwajengea uwezo wataalamu waliyopo katika Hospitali za Rufaa za Kanda pamoja na Hospitali za Rufaa za Mikoa hususan huduma za mkoba kwa kuwa Taasisi hiyo ni kituo cha umahiri wa Masuala ya Saratani nchini Tanzania.

Vilevile, aliitaka Taasisi hiyo kuharakisha harakati za kufungua vituo katika Mkoa wa Mbeya na Dodoma ili watu wanaotaka kupata huduma za mionzi wazipate kwa haraka.

Waziri Ummy aliipongeza Taasisi hiyo kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa huduma za Saratani kwa Watanzania na amewahakikishia kuwa Serikali itatimiza wajibu wake ili wafanye kazi katika mazingira rafiki.
Mwisho Alitoa wito kwa Watanzania kuwa na tabia ya kupima Afya zao mara kwa mara ili kujua hali zao za kiafya mapema na kuanza kupata huduma mapema kama umekutwa na ugonjwa ikiwemo Saratani.



# Zaidi ya familia 760 hanang zapatiwa elimu ya kujikinga na magonjwa ya mlipuko.



**Na Englibert Kayombo**
**Hanang, Manyara**

Serikali imesema Wahudumu wa Afya ngazi ya Jamii walitoa elimu kwa Familia zaidi ya 760 juu ya kutumia dawa ya kutibu maji ili kuzuia Magonjwa ya mlipuko kipindi hiki cha maafa katika mji mdogo wa Katesh Wilaya ya Hanang Mkoani Manyara.

Hayo yalisemwa Wilayani Hanang na Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel wakati akizungumza na Waandishi wa habari baada ya kufanya kikao cha kuwashukuru Wadau pamoja na watu wengine ambao wamekuwa bega Kwa bega na Serikali katika utoaji wa huduma na misaada kwa Waathirika wa Mvua ya Mafuriko.

"Tumeleta dawa za kutibu maji, katika kuhakikisha tunaimarisha suala la Kinga dhidi ya Magonjwa ya mlipuko tayari Wahudumu wa Afya wamefikia familia 760 kutoa elimu namna ya Matumizi ya dawa ya kutibu maji na hii itasaidia kwenye suala la kuzuia Magonjwa yatokanayo na maji ikiwemo kuhara hivyo tumejipanga Ili suala hili la Mafuriko lisilete balaa jingine". Alisema Dkt. Mollel.

Aidha, Dkt. Mollel alisema asilimia 98% ya Majeruhi ambao ilitakiwa wakatiwe rufaa wametibiwa ndani ya Mkoa wa Manyara hii ni kutokana na Serikali kujipanga vyema kuhakikisha kuwa huduma za kibingwa zimeimarishwa ili kuokoa uhai.

"Huduma za kibingwa zimesogezwa hapa, timu ya Madaktari bingwa wameweka Kambi mkoa wa Manyara ambapo asilimia 98 ya Wagonjwa waliotakiwa wakati Rufaa wanatibiwa hapa Manyara". Alisema.

Halikadhalika, Dkt. Mollel aliwashukuru Wadau kwa kuendelea kutoa ushirikiano katika kukabiliana na maafa yaliyotikea Katesh.

"Tunashukuru sana wadau na watu wengine kwa kuendelea kutoa ushirikiano yaani mmefanya kazi nzuri sana". Alisema.






# Doris Mollel Foundation yatoa vifaa tiba kwa ajili ya kuanzisha wodi ya watoto wachanga

**Na Hassan Kimweri**
**Tanga**

Taasisi ya Doris Mollel Foundation kwa kushirikiana na Msanii Barnabas ilitoa Vifaa Tiba kwa ajili ya kuanzisha Wodi ya Watoto Wachanga Mahututi (Neonatal Intensive Care Unit) ikiwemo watoto njiti katika Hospitali ya Masiwani, Halmashauri ya Jiji la Tanga.

Akipokea Vifaa hivyo, Mbunge wa Tanga Mjini na Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu alisema kuwa, mwelekeo wa Serikali ya awamu ya sita kwa Upande wa Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto ni kujikita katika utoaji wa huduma bora kwa watoto wachanga hususani watoto wanaozaliwa kabla ya wakati (njiti) ili kupunguza vifo vya watoto wachanga.

Mheshimiwa Ummy Mwalimu aliipongeza na kuishukuru Taasisi ya Doris Mollel Foundation kwa kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu za kuhakikisha Tanzania inafikia Malengo Endelevu ya Milenia ya kupunguza vifo vya watoto wachanga hadi kufikia vifo 12 kwa kila vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2030 kutoka vifo 24 kwa kila vizazi hai 1,000 kwa sasa.

Vifaa Tiba hivyo vimetolewa kwa lengo la kupunguza rufaa na kuwasaidia watoto hao kupata huduma bora karibu na jamii alipozaliwa kama alivyoeleza Mkurugenzi wa Taasisi ya Doris Foundation Bi Doris Mollel. Kulingana na tafiti mbalimbali zimeonesha kuwa watoto wachanga karibu asilimia 50 hupoteza maisha wanaposafirishwa umbali mrefu kwa sababu ya kupoteza joto la mwili.

Vifaa hivyo ni pamoja na Vitanda vya hospitali (2), Mashine ya mwanga ya kutibu manjano (1), Mashine ya kusaidia mtoto mchanga kupumua (1), Puto la kumsaidia mtoto kupumua (1), Mashine ya joto (1), Magodoro ya kuongeza joto la mtoto (10), Mashine za kutolea dawa kusaidia kupumua (3), Mashine ya kupima kiwango cha oxygen kwa mtoto (1),. Pump za miguu (5), Pump zaa umeme (3), Mashine za kutengeneza oxygen (2) na mizani ya kupima uzito wa watoto (2) vyenye thamani ya Tsh. Mil 35,000,000/=




# Rais Samia kuendelea kuimarisha huduma za afya mipakani

**Na. Majid Abdulkarim, Kilimanjaro**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt, Samia Suluhu Hassan amegawa magari 16 na Pikipiki 20 yakiwemo magari matatu ya kubebea wahisiwa wa magonjwa ya kuambukiza ili kutatua changamoto ya usafiri kwa watumishi na kuongeza kasi ya huduma maeneo ya mipakani na viwanja vya ndege nchini.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel katika hafla ya kukabidhi magari na pikipiki kwa ajili ya kuimarisha huduma za Afya mipakani katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro, Mkoani Kilimanjaro

Dkt. Mollel alisema Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan chini ya Wizara ya Afya imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za kudhibiti magonjwa kuenea ndani ya nchi yetu na kuzuia yasiingie au kuenea nje ya mipaka ya nchi.

“Hatua hii ni muhimu ili kutimiza Dira ya Sekta ya Afya ya kuwa na jamii yenye Afya inayochangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi binafsi na uchumi wa nchi kwa ujumla”. Alisisitiza Dkt. Mollel

Aidha, alibainisha kuwa uwekezaji wa Rais Samia nchini ni jitihada za ukuaji wa uchumi Kitaifa na Kimataifa zinachochea ongezeko la safari za abiria na mizigo kutoka eneo moja hadi eneo jingine.

Kwa wastani jumla abiria 114,000 kwa mwezi huwasili nchini kutoka nchi mbalimbali na pia wastani wa abiria 86,800 kwa mwezi husafiri nje ya nchi hasa kupitia uwanja wa ndege JNIA, Kiwanja cha ndege Kilimanjaro (KIA) pamoja na mipaka ya Namanga, Tunduma, Rusumo, Kasumulu na Mutukula.

Kwa kuzingatia umuhimu huo Wizara ya Afya inaendesha huduma za Afya katika mipaka 54 inayojumuisha Viwanja vya ndege 13, Bandari 12 na Mipaka ya nchi kavu 29.

Huduma zinazotolewa katika ofisi za Afya katika mipaka ni pamoja na Chanjo ya homa ya manjano, upimaji wa afya za abiria, ukaguzi wa vyombo vya usafiri pamoja na ukaguzi wa bidhaa mbalimbali ili kudhibiti kuenea kwa magonjwa.



# Rais Samia kuwezesha wananchi wengi kufikiwa na huduma za kibingwa na bingwa bobezi

**Na. Majid Abdulkarim,**
**Siha, Kilimanjaro**

Serikali chini ya Uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan imetenga kiasi cha shilingi Trilioni 6.7 kwaajili ya kuboresha Huduma za Afya ikiwa ni pamoja na kusomesha wataalamu ndani na nje ya nchi ili wananchi wengi waweze kupata matibabu ya kibingwa ya magonjwa mbalimbali yakiwemo ya Moyo.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Afya Dkt. Godwin Mollel wakati akiongea na wananchi waliofika katika Hospitali ya Wilaya ya Siha kwaajili ya kupata huduma za kibingwa za uchunguzi na Matibabu ya Moyo zinazotolewa na wataalamu wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) kwa kushirikiana na wenzao wa hospitali hiyo.

Dkt. Mollel ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Siha alisema katika kambi hiyo kwa muda wa siku tatu wataalamu wameona watu 307 kati yao 37 wamekutwa na matatizo yanayohitaji matibabu ya kibingwa na hivyo kupewa rufaa ya kwenda kutibiwa katika Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete.

"Kama hawa watu waliogundulika kuwa na matatizo wasingeonwa katika kambi hii si ajabu wasingeweza kuishi muda mrefu lakini uwepo wa matibabu haya umewasaidia kugundulika kuwa na matatizo ambayo yanahitaji matibabu ya kibingwa na watapata matibabu mapema", alisema Dkt. Mollel.

"Huduma za matibabu zinazopatikana katika upimaji huu zinatolewa bila malipo yoyote yale kwani Serikali imegharamia kila kitu na kutokana na uhitaji kuwa mkubwa JKCI wameongeza siku mbili hivyo basi kambi hii itamalizika siku ya Jumapili, ninawaomba wananchi mjitokeze kwa wingi kuja kupima afya zenu", alisisistiza Dkt. Mollel.

Dkt. Mollel alimshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuboresha huduma za Afya na hivyo kuwafanya watanzania na ambao siyo watanzania kuwa na uhakika wa kupata matibabu ya kibingwa na ndiyo maana Tanzania inapokea wagonjwa kutoka nchi za jirani ambao wanakuja kutibiwa hapa nchini.

Akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Dkt. Peter Kisenge, Mkurugenzi wa Tiba Shirikishi wa JKCI Dkt. Delilah Kimambo alisema Taasisi hiyo imekuwa ikitoa huduma ya Tiba mkoba ijulikanayo kwa jina la Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Outreach Services ya kuwafuata wananchi mahali walipo na kutoa huduma za kibingwa za matibabu ya Moyo.

# Tanzania yavunja rekodi matibabu ya Moyo

**Na. Said Nyaoza**
**Dar es salaam**

Upasuaji mdogo wa Moyo wa kubadilisha valvu ya mshipa mkubwa wa Damu (Aortic Valve) bila kufungua kifua (Transcatheter Aortic Valve Implantation procedure – TAVI)

Upasuaji huo wa historia ulifanyika kwa wagonjwa watatu wenye umri wa zaidi ya miaka 70 katika kambi maalumu ya matibabu ya siku mbili iliyofanywa na wataalamu wa magonjwa ya Moyo na mishipa ya damu wa JKCI na wenzao wa Hospitali ya Starcare ya nchini India.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. John Jingu alisema uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali katika Sekta ya Afya hii ikiwa ni pamoja na kujenga majengo ya kisasa, kusomesha wataalamu na kuunua vifaa tiba vya kisasa kumewezesha kufanyika kwa upasuaji huo.

Dkt. Jingu alisema kutokana na umuhimu mkubwa wa sekta ya Afya Serikali itaendelea kuboresha huduma ya afya ikiwa ni pamoja na kusomesha wataalamu katika nchi mbalimbali ambao watakuja kutoa matibabu ya kibingwa nchini.

Kwa Julai hadi Disemba mwaka huu alidokeza kuwa JKCI imehudumia zaidi ya wagonjwa 3,000 katika kufanya upasuaji mkubwa na mdogo wa Moyo na kusisitiza Serikali itaendelea kuhakikisha Wananchi wanapata huduma za kibingwa za Matibabu.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) Dkt. Peter Kisenge aliishukuru Serikali kwa kuiwezesha Taasisi hiyo ambayo imeweza kufanya matibabu hayo ya kihistoria ambapo kwa nchi za Afrika hakuna hospitali ya Serikali inayotoa huduma hiyo.

“Serikali ya awamu ya sita imetuwekea vifaa vingi ambavyo vimewezesha Wagonjwa wa namna hii ambao ni wengi na walikuwa hawajui waende kutibiwa wapi kufanyiwa matibabu, hata wenzetu walifurahia aina ya vifaa tulivyonavyo ambavyo vimewawezesha wataalamu wetu kufanya upasuaji wenyewe kwa asilimia 90”,alisema Dkt. Kisenge.

Aidha Dkt. Kisenge alisema JKCI imeendelea kuwa kituo cha utalii tiba ambapo wagonjwa kutoka nchi 20 za Afrika zinafika kwenye taasisi hiyo kupata matibabu kutokana na wingi wa wagonjwa, aliiomba Serikali jengo lingine kwaajili ya kuwahamishia wagonjwa ombi ambalo Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Dkt. Jingu alisema linafanyiwa kazi.





# Mtambo wa kutibu magonjwa zaidi ya 10 wazinduliwa Muhimbili

**Na. Shaban Juma**
**Dar Es Salaam**

Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imezindua Mtambo unaotumia Hewa Tiba yenye mgandamizo ya Oksijeni (Hyperbaric Medicine Treatment) ambao unatibu magonjwa zaidi ya 10 na kuifanya Tanzania kuwa nchi ya kwanza katika Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na ya pili Kusini mwa Jangwa la Sahara kutumia mtambao huo uliogharimu Tsh. Milioni 250.

Akizungumza katika hafla ya ufunguzi wa mtambo huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili Prof. Mohamed Janabi alisema kupitia matibabu haya mgonjwa huingizwa kwenye kifaa maalumu na kupatiwa tiba kupitia hewa tiba ya Oksijeni iliyogandamizwa kwa 100%.

Aliyataja wagonjwa watakaonufaika kuwa ni wale wenye vidonda sugu ambavyo matibabu mengine yameshindikana kama wagonjwa wa Sukari (Diabetic Foot), walioathirika na moshi baada ya kuungua na moto (Carbon Monoxide Poisoning) na waliopata changamoto za upungufu wa oksijeni mwilini kama waliozama kwenye maji baharini n.k (Decompression Syndrome).

Prof. Janabi alisema wagonjwa wengine ni pamoja na walioungua na moto (Acute Thermal Injury), wenye upungufu mkubwa wa damu ambao kwa njia moja au nyingine hawawezi kuongezewa damu (Severe Anemia), waliopata ajali na kupata majeraha mwilini yasiyopona (Crush Injury, Compartment Syndrome and other Acute Traumatic Ischemia) na wagonjwa wenye maambukizi kwenye mifupa isiyopona (Refractory Osteomyelitis)

Aliongeza kuwa wagonjwa wengine waliopata mionzi na kusababisha sehemu zilizopata tiba mionzi kuathitika ikiwemo wenye Saratani za Koo, njia ya chakula na wale wenye Tezi Dume (Delayed Radiation Injury both soft tissue and bony necrosis), waliofanyiwa upasuaji na kuwekewa/kupandikiziwa sehemu ya miili yao (Compromised Grafts and Flaps), wenye changamoto ya kusikia ambao vipimo vimeshindwa kuonyesha tatizo (Idiopathic Sudden Sensorineural Loss), wenye tatizo la Usaha kwenye Ubongo (Intracranial Abscess), wenye changamoto ya oksijeni kwenye Mishipa ya Damu (Arterial Insufficiencies) na watoto wenye Usonji (Autisim).

Prof. Janabi aliishukuru Kampuni ya Sechrist ya nchini Marekani ambao ndio watengenezaji na ndiyo waliotoa msaada huo wenye thamani ya Tsh. Milioni 250.




# Wabunifu wa huduma za afya za kidigitali wahimizwa kuboresha huduma bora za afya kupitia tehama

**Na. Cletus Sanga,**
**Dar Es Salaam.**

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dkt. John Jingu amewahimiza wabunifu wa Huduma za Afya za Kidigitali kushirikiana na Serikali ili kuweza kuboresha huduma bora za kiafya kwa wananchi kupitia TEHAMA.

Dkt. Jingu aliyasema hayo katika Jukwaa la Wabunifu wa Afya ya Kidijitali lililofanyika katika Ukumbi wa Mwalimu Julius Nyerere Disemba 18, 2023 lililohudhuriwa na wadau mbalimbali kama vile Mamlaka ya Serikali Mtandao (EGA) na wadau Sekta binafsi nchini.

"Tunafahamu kwamba dunia ya sasa ni ya teknolojia na teknolojia za kidigitali. Serikali, kupitia Wizara ya Afya, imeweka mikakati mbalimbali kutumia teknolojia za kisasa katika kuboresha utoaji wa huduma za Afya". Alisema Dkt. Jingu.

Aidha, Dkt. Jingu alisema Serikali, kupitia Wizara ya Afya, imeongeza kasi ya utoaji wa huduma bora za Afya kwa wananchi kwa kutumia teknolojia za kidigitali. Teknolojia hizi zimeweza kusaidia kutoa huduma bora kwa haraka, ufanisi, kasi na usahihi zitakazoruhusu upatikanaji wa huduma za Afya kwa urahisi.

Pia, Dkt. Jingu alisema Wizara ya Afya imeanzisha Kituo cha Afya cha Kidijitali (CDH) yenye lengo la kuhakikisha wadau wote kwenye sekta ya Afya wanafanya kazi kwa pamoja na wanapata njia wanayoweza kushirikiana katika kutatua changamoto zilizopo katika sekta ya afya ili kuboresha huduma za Afya nchini.

"Teknolojia italeta mapinduzi makubwa, na mapinduzi haya yanawezekana, kama tutaweza kufanya kazi kwa pamoja". Alisema Dkt. Jingu.



# Umoja wa wamiliki vituo binafsi vya afya (APHTA), wapitishwa kwenye sheria ya bima ya afya kwa wote

**Na. Said Nyaoza**
**Dar Es Salaam**

Mkurugenzi Msaidizi wa Mipango na Bajeti wa Wizara ya Afya Bw. Lusajo Ndagile, amewapitisha kwenye Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote Umoja wa Wamiliki wa Vituo Binafsi vya Afya nchini (APHTA) ili kupata maoni yao maeneo ambayo yanaweza kufanyiwa maboresho kabla ya kuanza utekelezaji wake.

Bw. Lusajo aliyasema hayo wakati wa kikao cha kupitia Sheria ya Bima ya Afya kwa wote kilichofanyika kwenye Ofisi ndogo za wizara ya Afya jijini Dar es Salaam.

“Sisi kama Wizara ya Afya na kama Serikali jukumu letu kubwa ni kupokea maoni yenu ili kile tulichokifanya tuweze kukiboresha na mwisho wa siku tuweze kumsaidia Mwananchi katika kupata huduma bora za Afya na zenye ufanisi”. Alisema Lusajo.

Aidha Bw. Lusajo alisema Wizara ya Afya iko kwenye mchakato wa kukutana na wadau mbalimbali wa Afya na kuwapitishia kwenye sheria ya Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote ambayo ilisainiwa hivi karibu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na kupokea maoni ya wadau hao, kwa ajili ya maboresho mbalimbali kabla ya kuanza utekelezaji wake.

Akizungumza kwa niaba ya APHTA Mwenyekiti wa Umoja huo Bw. Mahmoud Mringo, aliipongeza Wizara ya Afya kwa kutambua umuhimu wao, na kuwapa fursa ya kuweza kutoa maoni yao kabla ya kuanza utekelezaji wake.

“Fursa hii sisi tumeipigania kwa muda mrefu, na kuzaliwa kwa mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote kwetu ni faraja kubwa, hivyo tunategemea kupitia kikao hiki tunategemea ule usisi na uwao utaondolewa na hatimaye tunaenda kuwahudumia Watanzania kwa haki na usawa”.Alisema Mringo.

Pia, Bw. Mringo aliiomba Wizara ya Afya na wote watakaohusika na utekelezaji wa mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote, kuhakikisha wanafanyia kazi changamoto ambazo Vituo vyao vya Afya vilikuwa vikikutana nazo wakati wa utekelezaji wa Bima ya Afya iliyopo, na kuhakikisha ujio wa Bima ya Afya kwa wote utekelezaji wake unakuwa ufanisi mkubwa.

# Muhimbili yapeleka msaikolojia tiba katesh na msaada wa dawa za tzs. 38 mil

**Na, Englibert Kayombo**
**Hanang, Manyara**

Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) imeungana na wananchi wa Mji mdogo wa Katesh Wilayani Hanang, Mkoani Manyara na kupeleka msaada wa Dawa na Vifaa Tiba vyenye thamani ya Tsh. milioni 38 ili kusaidia jitihada za utoaji huduma katika eneo hilo, ambalo hivi karibuni lilikumbwa na maafa ya mafuriko yaliyosababisha maporomoko ya udongo kutoka mlima Katesh na kuleta madhara makubwa ikiwemo vifo, majeruhi, upotevu wa mali na uharibifu wa miundombinu.

Akizungumza kwa Niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Mkuu wa Idara ya Famasi, Mfamasia. Nelson Faustine alisema sambamba na msaada huo, Hospitali imetuma Msaikolojia Tiba kwenda kuungana na timu za watalam mbalimbali walioko kule wanaotoa huduma kwa waathirika wa mafuriko hayo.

wenyewe wamesifia lakini pia nimeona watoa huduma wakifanya kazi zao vizuri, nawapongeza sana kwa hili." Alisema Dkt. Jingu

Hatua hii pia ni kuitikia wito wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye aliagiza kupelekea Watalaam wa Saikolojia kuzungumza na wananchi waliopata mfadhaiko kutokana na tukio hilo ili waweze kurejea katika hali ya kawaida.

Bodi ya Wadhamini, Menejimenti na Wafanyakazi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili wanaendelea kutoa pole kwa wananchi wa Mji mdogo wa Katesh Wilayani Hanang, Mkoani Manyara kutokana na madhara waliyopata.



# Wataalamu wa huduma za dharura za mama na mtoto wachanga watakiwa kuwezesha matumizi bora ya vifaa



**Na. Abdulwaheed Madenge, Dodoma.**

Wataalamu wa afya waliohudhuria Mafunzo elekezi ya Huduma za dharura ya Uzazi na Watoto wachanga (EmONC) wametakiwa kuwezesha Vituo vya Afya kuona umuhimu matumizi bora ya vifaa na kuanzisha huduma mpya ambazo zitawasaidia kuokoa Maisha ya Mama na Mtoto.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa huduma za mama na mtoto Dkt. Ahmad Makuwani wakati wa Mafunzo elekezi ya wataalamu wa (EmONC mentorship) Kampeni ya Mama Samia iliyofanyika jijini Dodoma.

Dkt. Makuwani alisema kuwa Mafunzo hayo yawe chachu ya kuwafanya wataalamu hao kwenda kutumia ujuzi walionao katika kuboresha huduma za mama na mtoto ili kuendelea kuzuia Vifo vya mama na mtoto.

Aidha Dkt. Makuwani alisema kuwa kupitia Mafunzo hayo wanatarajia kuona baadhi ya huduma zinafika mahala pake kwa kutumia njia za kujifunzia ambazo hazibadiliki katika Nyanja ya Mafunzo.

"Hizi steps of learning huwa hazibadiliki, hivyo tunatarajia kuona baadhi ya product zinafika mahali pake, ni muhimu mkaoneshe umuhimu wa matumizi ya vifaa na sio kukaa stoo".

Aidha Dkt. Makuwani aliwaasa wataalamu hao kutumia lugha zenye staha ili kuboresha huduma na si kutumia lugha za ukali kwani lengo la kampeni ni kujifunza na kuboresha Huduma za mama na mtoto.

# UGONJWA WA KISUKARI UNAZUILIKA

Pima SUKARI mara kwa mara

## Kwa Kuzingatia yafuatayo

- Punguza uzito uwiane na urefu wako
- Punguza Chumvi, Sukari na Mafuta. Ongeza kiasi cha Matunda na Mbogamboga
- Fanya Mazoezi angalau Nusu Saa Kila Siku




**Jarida hili limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**WIZARA YA AFYA, TANZANIA, TOLEO LA MWEZI DISEMBA, 2023**